

BODI YA WATAALAM WA UNUNUZI NA UGAVI

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

UTANGAZAJI WA MATOKEO YA MITIHANI YA 28 YA PSPTB

Dar Es Salaam, Julai 19, 2024.

Bodi ya Wataalam wa Ununuizi na Ugavi (PSPTB) inapenda kutangaza rasmi matokeo ya mitihani ya 28 ya PSPTB iliyofanyika kuanzia 13 Mei hadi 17 Mei, 2024 katika vituo sita vya mitihani Tanzania bara na Visiwani.

Jumla ya watahiniwa wapatao 1,280 walisajiliwa ili kufanya mitihani hii ambapo watahiniwa 1,197 (93.5%) walifanya mitihani hii ikiwa ni ongezeko la watahiniwa ukilinganisha na msimu uliopita ulikuwa na watahinwa 977.

Taarifa ya matokeo ya mitihani ya 28 ya PSPTB ni kama ifuatavyo:

- (a) Kati ya watahiniwa 1,280 Jumla ya watahiniwa 551 sawa na 46.0% wamefaulu mitihani yao, watahiniwa 632 sawa na 52.8% watarudia baadhi ya masomo kuanzia somo moja mpaka masomo matatu kutegemeana na masomo idadi ya masomo aliyofeli, na watahiniwa 14 sawa na 1.2% wamefeli masomo yote waliyofanya katika ngazi zao.
- (b) Katika masomo 39 waliyopimwa watahiniwa, masomo 24 yalifanywa vizuri, 07 yalifanywa kwa wastani na masomo 08 yalikuwa chini ya wastani;
- (c) Kwa ujumla watahiniwa **wa kike** walifanya vizuri ukilinganisha na watahiniwa wa kiume. Katika ufaulu wa jumla watahiniwa wawili wakike wakiibuka watahiniwa bora katika ngazi za mitihani za Graduate Professional I, na CPSP.

Mikakati ya PSPTB kwa siku za mbele

- (a) Kuendelea kuimarisha na kusimamia ubora wa mafunzo yanayotolewa na vituo vyta kuwaandaa watahiniwa – review centers
- (b) Kuendelea kuimarisha mahusiano ya kitaaluma na Taasisi za elimu ya Juu na Kati ili kuongeza ubora na ufaulu katrika mitihani ya PSPTB,
- (c) Kuendelea kuhimiza na kusimamia uanzishwaji na uendeshaji wa mafunzo kwa kutumia fursa ya nyezo za mitando zilizopo.
- (d) Kuendelea kufanya ziara za kimafunzo vyuoni na katika vito vyta mafunzo vilivyosajiliwa na PSPTB ili kuhamasisha usomaji wenye tija kwa ajili ya utendaji mzuri katika mitihani ya PSPTB,
- (e) Kuendelea kutembelea vyuo mbalimbali vinavyofundisha taaluma ya Ununuzi, Ugavi, Usafirishaji , kushiriki maonesho mbalimbali yakiwemo ya kitaaluma na kutoa aelimu ya umuhimu wa kufanya mitihani ya PSPTB.

Imetolewa na :

Godfred B. Mbanyi

Mkurugenzi Mtendaji - PSPTB